**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**
**2020 - 2025**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Zubeir Ali Maulid | - | SPIKA |
| 2. | Mhe. Mgeni Hassan Juma | - | Naibu Spika/Nafasi za Wanawake |
| 3. | Mhe. Hemed Suleiman Abdulla | - | MBM/Makamu wa Pili wa Rais//Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Uteuzi wa Rais |
| 4. | Mhe. Abdalla Hussein Kombo | - | Jimbo la Mkoani |
| 5. | Mhe. Abdalla Abass Wadi | - | Jimbo la Nungwi |
| 6. | Mhe. Ali Abdulghulam Hussein | - | Jimbo la Jang'ombe |
| 7. | Mhe. Ali Suleiman Ameir | - | Jimbo la Pangawe |
| 8. | Mhe. Ameir Abdalla Ameir | - | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 9. | Mhe. Anna Athanas Paul | - | Uteuzi wa Rais |
| 10. | Mhe. Asha Abdalla Mussa | - | Jimbo la Mahonda |
| 11. | Mhe. Aza Januar Joseph | - | Nafasi za Wanawake |
| 12. | Mhe. Bahati Khamis Kombo | - | Jimbo la Chambani |
| 13. | Mhe. Bakari Hamad Bakari | - | Jimbo la Wawi |
| 14. | Mhe. Bihindi Hamad Khamis | - | Nafas iza Wanawake |
| 15. | Mhe. Fatma Ramadhan Mohamed (Mandoba) | | Nafasi za Wanawake |
| 16. | Mhe. Habibu Ali Muhamed | - | Jimbo la Mtambwe |
| 17. | Mhe. Haji Omar Kheri | - | Jimbo la Tumbatu |
| 18. | Mhe. Haji Shaaban Waziri | - | Jimbo la Uzini |
| 19. | Mhe. Hamza Hassan Juma | - | Jimbo la Kwamtipura |
| 20. | Mhe. Haroun Ali Suleiman | - | Jimbo la Makunduchi |
| 21. | Mhe. Harusi Said Suleiman | - | Jimbo la Wete |
| 22. | Mhe. Hassan Hamad Omar | - | Jimbo la Kojani |
| 23. | Mhe. Hassan Khamis Hafidh | - | Jimbo la Welezo |
| 24. | Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir | - | Nafasi za Wanawake |
| 25. | Mhe. Hussein Ibrahim Makungu | - | Jimbo la Mtoni |
| 26. | Mhe. Jamal Kassim Ali | - | Jimbo la Magomeni |
| 27. | Mhe. Juma Makungu Juma | - | Jimbo la Kijini |
| 28. | Mhe. Juma Ali Khatib | - | Uteuzi wa Rais |
| 29. | Mhe. Dkt Khalid Salum Mohamed | - | Jimbo la Donge |

30. Mhe. Issa Haji Ussi Gavu - Jimbo la Chwaka
31. Mhe. Kombo Mwinyi Shehe - Jimbo la Wingwi
32. Mhe. Lela Mohamed Mussa - Nafasi za Wanawake
33. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
34. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
35. Mhe. Masoud Ali Mohammed - Jimbo la Ole
36. Mhe. Mihayo Juma Suleiman - Jimbo la Mwera
37. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
38. Mhe. Mohamed Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
39. Mhe. Mohamed Ahmada Salum - Jimbo la Malindi
40. Mhe. Mudrik Ramadhan Suleiman - Jimbo la Bububu
41. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bubwini
42. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
43. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma - Jimbo la Dimani
44. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
45. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis - Nafasi za Wanawake
46. Mhe. Mwanajuma Kassim Makame - Nafasi za Wanawake
47. Mhe. Dkt. Mwinyi Talib Haji - Mwanasheria Mkuu
48. Mhe. Nadir Abdullatif Yussuf - Jimbo la Chaani
49. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
50. Mhe. Panya Ali Abdall - Nafasi za Wanawake
51. Mhe. Rahma Kassim Ali - Nafasi za Wanawake
52. Mhe. Riziki Pembe Juma - Nafasi za Wanawake
53. Mhe. Rukia Omar Ramadhan - Jimbo la Amani
54. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafas iza Wanawake
55. Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum - Uteuzi wa Rais
56. Mhe. Saidi Saleh Salim - Jimbo la Tumbe
57. 5Mhe. Sabiha Fil fil Thani - Nafasi za Wanawake
58. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
59. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
61. Mhe. Soud Nahoda Hassan - Jimbo la Paje
62. Mhe. Suleiman Masoud Makame - Jimbo la Chonga
63. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani

| | | | |
|---|---|---|---|
| **64. Mhe.** | **Suleima Haroub Suleiman** | **-** | **Jimbo la Kiembe Samaki** |
| **65. Mhe.** | **Sulubu Kidongo Amour** | **-** | **Jimbo la Mkwajuni** |
| **66. Mhe.** | **Shadya Mohamed Suleiman** | **-** | **Nafasi za Wanawake** |
| **67. Mhe.** | **Shaaban Ali Othman** | **-** | **Jimbo la Mpendae** |
| **68. Mhe.** | **Shamata Shaame Khamis** | **-** | **Jimbo la Micheweni** |
| **69. Mhe.** | **Shaib Hassan Kaduara** | **-** | **Jimbo la Chake Chake** |
| **70. Mhe.** | **Tabia Maulid Mwita** | **-** | **Uteuzi wa Rais** |
| **71. Mhe.** | **Yahya Rashid Abdulla** | **-** | **Jimbo la Kwahani** |
| **72. Mhe.** | **Yussuf Hassan Iddi** | **-** | **Jimbo la Fuoni** |
| **73. Mhe.** | **Zaina Abdalla Salum** | **-** | **Nafasi za Wanawake** |
| **74. Mhe.** | **Zawadi Amur Hassan** | **-** | **Jimbo la Konde** |

| | | |
|---|---|---|
| **Ndg. Raya Issa Msellem** | **-** | **Katibu** |

**Kikao cha Pili – Tarehe 10 Novemba, 2020**

*(Kikao kilianza saa 8:00 mchana)*

## DUA

*Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma dua*

## TAARIFA YA RAIS

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe naomba kuanza kwa kutoa taarifa ya Ujio wa Mhe. Rais. Taarifa hii ni rasmi, imeletwa kwa barua rasmi na naomba niisome mbele yenu, ni Taarifa ya Mhe. Rais kulihutubia Baraza la Wawakilishi.

Kwa heshima naomba uhusike na mada ya hapo. Kwa kuzingatia Masharti ya Kanuni ya 21(9) nimeagizwa na Mhe. Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, nikuarifu kwamba anakusudia kutoa Hotuba ya Ufunguzi wa Baraza la 10 la Wawakilishi, siku ya Jumatano, Tarehe 11 Novemba, 2020 saa 9:00 za alasiri.

Kwa hivyo, kwa barua hii, hii ndio imekuwa Taarifa Rasmi ambayo nimeisoma mbele yenu ili sasa muweze kuelewa kwamba tunatarajia kuwa na ujio wa Mhe. Rais, na siku hiyo kwa kweli ni kesho.

Baada ya kusoma taarifa hiyo, naomba sasa nirudi tena kwa Katibu shughuli inayofuata.

## UCHAGUZI WA NAIBU SPIKA

**Mhe. Spika:** Waheshimiwa Wajumbe kama tunavyofahamu juzi hapa tumefanya kazi nzuri sana ya kumpata Spika. Lakini bila shaka Spika huyo atahitaji wasaidizi, na mmoja katika wasaidizi ni Naibu Spika. Kwa hivyo, leo tutafanya kazi ya kumpata Msaidizi Mkuu wa Spika, na baada ya hapo, sio leo, tutafuata hatua nyengine za kuwapata Wenyeviti kwa ajili ya usaidizi wa uendeshaji wa shughuli hizi za Baraza. Na kwa ufupi kabisa, sasa naomba nimwite Katibu ili atupe utaratibu na atuongoze katika utaratibu huu wa upatikanaji wa Naibu Spika. Katibu karibu sana.

**Katibu:** Mhe. Spika, utaratibu wetu wa kumpata Mhe. Naibu Spika utakuwa kwa mujibu wa Kanuni ya 8. Na utaratibu huo unaelekezwa kwamba utakuwa kama Uchaguzi wa Kumchagua Spika wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, kwa hivyo hatua ya kwanza ni kumwita mgombea. Na Ofisi ya Katibu imepokea jina la mgombea mmoja pekee kutoka Chama cha Mapinduzi ambaye ni Mhe. Mgeni Hassan Juma. Na kwa mujibu wa taratibu ni kwamba, Mhe. Spika kiti chako kitamwita Mhe. Mgeni Hassan Juma ili kuomba kura kwa Waheshimiwa Wajumbe kwa muda usiozidi dakika tano na baada ya hapo, Waheshimiwa Wajumbe watakuwa na nafasi ya kuuliza maswali yasiyozidi matatu na baadae zoezi la kupiga kura litafanyika. Na Mhe. Mgombea ana nafasi ya kuchagua wakala au kushuhudia zoezi la kuhesabu kura yeye mwenyewe. *(Makofi)*

Kwa hivyo, wakati ambapo anakuja kutoa hotuba yake ya kuomba kura ataeleza kama atateuwa wakala au atashuhudia mwenyewe zoezi la kuhesabu kura. Kwa hivyo, Mhe. Spika, naomba kwa heshima nikabidhi kwako ili uweze kuendelea na utaratibu wa kumwita Mgombea wa Kiti cha Naibu Spika ili aweze kujieleza na baadae kuomba kura na zoezi la uchaguzi liendelee.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wajumbe sasa kwa heshima na taadhima naomba nimkaribishe Mhe. Mgeni Hassan Juma ili aje ajieleze na kama alivyoelezwa hapa awali, atakuwa na dakika zisizozidi tano za kujieleza na kama kutakuwa na maswali yasiyozidi matatu ataulizwa. Mhe. Mgeni Hassan Juma karibu sana. *(Makofi)*

**Mhe. Mgeni Hassan Juma:** Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, awali ya yote nichukue fursa hii adhimu kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema ambaye ametujaalia leo hii kuja hapa tukiwa wazima wa afya na kuweza kuendelea na shughuli ambayo tumejipangia.

Mhe. Spika, lakini pia nikushukuru wewe na ofisi yako kwa kunipa fursa hii ya kuweza kujielezea machache ambayo yanatokana na mustakabali ambao tuimeupanga wa Kikanuni zilizokuwemo ndani ya Baraza na Katiba.

Mhe. Spika, mimi kwa jina naitwa Mgeni Hassan Juma. Nadhani wengi waliokuwepo hapa wananifahamu, kuna ambao nimefanya nao kazi kuanzia mwaka 2010 mpaka 2015 na wengine wapo hapa nimefanya nao kazi kuanzia 2015 mpaka 2020, na ninafahamu vizuri sana kuna wengine wapya, lakini hata hivyo tumefanya kazi katika maeneo mbali mbali, yakiwemo katika Chama chetu cha  Mapinduzi.

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa sana na unyenyekevu mkubwa sana, naomba Wajumbe pamoja na wewe Mhe. Spika mnipe kura zenu ili niendelee kufanya kazi ya Unaibu Spika ambayo nimeifanya kwa kupindi cha miaka mitano. Ninachoahidi kwenu nitatenda haki na nitakuwa muadilifu na nitakuwa na mashirikiano makubwa na Wajumbe wote pamoja na Watendaji wote wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, naomba kura, naomba kuwasilisha. Ahsante sana. (*Makofi)*

**Mhe. Spika:**  Ahsante sana Mhe. Mgeni Hassan Juma, Waheshimiwa Wajumbe kama kuna maswali. Maswali, maswali.

Ahsante sana Mhe. Mgeni Hassan Juma unaweza kurudi kwenye kiti chako.

**Katibu:** Mhe. Spika, kabla ya kuanza zoezi la kupiga kura, ofisi yetu imewahesabu Wajumbe waliomo ndani ya Ukumbi wa Baraza na imepata jumla ya Wajumbe 67. Kwa hivyo, kabla ya kugawa kura, tuliona ni vyema kujiridhisha kwanza idadi ya wajumbe waliopo, na kwa hivyo tutagawa kura 67.

Mhe. Spika, baada ya hayo tunaomba ridhaa yako ili tuweze kuanza kugawa kura kwa Waheshimiwa Wajumbe.

**Mhe. Spika:** Ahsante. Tulipofunga hesabu natumai hakuna mjumbe yeyote mpya ambaye ameingia. Kama hakuna, ningemuomba Mhe. Mgombea kama ana mtu ambaye anataka kuwa wakala wake. Mhe. Mgeni Hassan Juma kwanza tupe wakala, halafu turuhusu zoezi lianze.

**Mhe. Mgeni Hassan Juma:** Namchagua Mhe. Panya Ali Abdalla.

**Mhe. Spika:** Ahsante sana, Mhe. Panya Ali Abdalla atamuwakilisha Mheshimiwa. Ninaruhusu sasa kura zianze kugaiwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, masanduku yatapitishwa hapo hapo ili kutokupeni usumbufu. Lakini ningependa pia hawa wenye masanduku wayaoneshe kuthibitisha kwamba hayana kitu ndani, na hilo jengine pia na lenyewe, ahsante.

Haya, kama tayari naomba sasa kura zianze kukusanywa. Waheshimiwa hakikisheni kura zenu zina muhuri nyuma. Kama kuna yeyote amefanya kosa kwenye kura yake na atahitaji kuibadilisha pia naweza kuarifiwa.

Watu wote wameshatumbukiza kura kwenye kisanduku. Kama wameshakamilika tunaomba visanduku vije huku mbele, kuna yeyote ambaye amebaki, kuna mjumbe mwengine yeyote zaidi ya Spika ambaye amebaki na kura.

Nashukuru sana, sasa naomba nimwite Mhe. Panya Ali Abdalla. Na hili zoezi Waheshimiwa Wajumbe kwa sababu ya idadi yetu tunashauri lifanyike hapa hapa tu mbele mezani. Kwa hivyo, Mhe. Panya Ali Abdalla njoo hapa mbele, ni zoezi la wazi, lakini wakati huo huo kwa sababu halitachukua muda mrefu, naomba wajumbe tubaki humu humu ndani ya Ukumbi na baadae tutatangaza hayo matokeo ili tuweze kwenda kwenye shughuli nyengine inayofuata. Mhe. Panya Ali Abdalla karibu sana.

*(Saa 8.15 mchana Baraza liliakhirishwa mpaka baada ya kuhesabu kura)*

*(Saa 8:20 mchana Baraza lilirudia)*

**Mhe. Spika:** Katibu karibu kwa matokeo.

**Katibu**: Ahsante Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba niendelee na zoezi linalofuata nalo ni baada ya kumaliza uchaguzi wetu na kufanya hesabu tunaomba tutoe matokeo ya uchaguzi wa Naibu Spika wa Baraza uliofanyika leo tarehe 10 Nevomba, 2020.

Mhe. Spika, maelezo ni kama yafuatayo:-

Wajumbe waliopiga kura kati ya Wajumbe wote waliohudhuria ni 67 sawa na asilimia mia. Kura halali ni 67 sawa na asilimia mia, kura zilizoharibika ni 0 na kura zilizomkubali Mhe. Mgeni Hassan Juma kutoka Chama cha CCM ni 67 sawa na asilimia mia. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hivyo Mhe. Mgeni Hassan Juma kutoka Chama cha Mapinduzi amechaguliwa kuwa Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi kwa kipindi cha mwaka 2020/2025 kwa kupata kura 67 sawa na asilimia mia ya kura zilizopigwa. Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Katibu kwa matokeo.

Waheshimiwa Wajumbe kwanza kabisa na mimi nichukue nafasi hii kuungana na nyinyi kumpongeza Mhe. Mgeni Hassan Juma kuwa ndiye Naibu Spika wetu kwa kuchaguliwa kwa asilimia mia moja ya kura zote zilizopigwa.

Baada ya hapo, sasa naomba nimkaribishe kama ana machache ya shukrani halafu tuweze kuendelea na shughuli nyengine. Mhe. Mgeni Hassan Juma, Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi karibu sana. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Spika, naomba nichukue fursa hii tena kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amejaalia kwamba leo tumepiga kura ya Naibu Spika, na *Alhamdulillah* kura hizi zote zimenikubali kwa asilimia mia moja. Namshukuru sana Mwenyezi Mungu.

Lakini Mhe. Spika, niwashukuru wajumbe wote kwa kunikubali na kunipigia kura za ndio, nawashukuru sana. Mhe. Spika, pia napenda kuishukuru familia yangu ambayo kwa kipindi chote pamoja na cha kampeni na kipindi hichi wamekuwa pamoja na mimi na kwa kweli wamenisaidia sana katika harakati mbali mbali wakati nikiwa katika shughuli zangu za kisiasa.

Nichukue fursa hii kumshukuru sana mume wangu yule pale juu Bw. Shukuru leo amekuja na yeye kuona namna gani mkewe anachaguliwa kuwa Naibu Spika, kwa hiyo nakushukuru sana kwa hilo.

Waheshimiwa Wajumbe, mimi nadhani sina mengi sana ya kusema. Isipokuwa nataka kuzungumza jambo moja tu ambalo naona lina umuhimu mkubwa sana.

Kwanza kabisa, naomba nichukue fursa hii nimshukuru sana Mhe. Mwanaasha Khamis Juma, nampongeza na namshukuru kwa sababu tumeingia katika kinyang’anyiro pamoja na kwa kweli hiyo ni demokrasia ya Chama cha Mapinduzi. Lakini amekuwa ni jasiri wa kuingia ndani ya kinyang`anyiro hichi akiwa anajua kwamba na yeye ana kila haki ya kugombea. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma nakushukuru na nakupongeza sana kwa hatua ambayo umefikia na Mwenyezi Mungu atakujaalia utafika mbele zaidi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, jengine ambalo nataka kulizungumza ni umoja, mashirikiano na upendo baina yetu ni muhimu sana waheshimiwa. Waheshimiwa Wajumbe, nasema hivyo ili kwamba tunapoanza Baraza letu leo hili tuanze tukiwa na upendo na mashirikiano makubwa. Sote ni wanachama wa Chama cha Mapinduzi kazi yetu ni moja ya kuhakikisha kwamba tunailinda serikali yetu lakini tunakilinda na chama chetu.

Niseme hayo machache Mhe. Spika, nakushukuru tena na nawashukuru watendaji wote wa Baraza la Wawakilishi kwa mashirikiano yao makubwa ambayo wamenipa. Niwashukuru sana watendaji wangu ndani ya ofisi yangu ambao nimefanya nao kazi kwa muda wa miaka mitano

kwa kweli wamenisaidia sana katika shughuli zangu zote. Nawashukuru sana Mhe. Spika, nakushukuru na wewe kwa kunilea kwa kunifundisha mpaka nimefikia hapa. Mhe. Spika, nashukuru sana, ahsante sana. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa hotuba yako fupi ya shukrani. Waheshimiwa Wajumbe, naomba sasa nimwite Mhe. Mwanasheria Mkuu ili tutengue hoja. Mhe. Mwanasheria Mkuu tafadhali.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Spika, naomba Baraza lako tukufu liridhie kuweka kando kanuni ya 23 inayohusiana na nyakati za vikao, ili kuweza kuruhusu kikao cha Baraza cha kesho tarehe 11/11/2020 kuanza saa 8:00 mchana badala ya muda ulioelezwa katika kanuni hiyo.

Mhe. Spika, vile vile naomba kuwekwa kando kwa kanuni ya 132 inayohusiana na ukaaji wa wajumbe ndani ya Baraza ili kuruhusu kuingia ukumbini Mhe. Spika wa Bunge la Afrika Mashariki, Mhe. Jaji Mkuu wa Zanzibar, Mke wa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, pamoja na walinzi wa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**Mhe. Spika:** Ahsante sana Mhe. Mwanasheria Mkuu. Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa na naomba sasa niwahoji, wale wote wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Mwanasheria Mkuu wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya kuweka kando kanuni kuna tangazo moja kabla hatujaakhirisha hizi shughuli zetu. Tangazo linatoka Chama cha Mapinduzi ambalo linawataka Waheshimiwa Wajumbe kwanza mnaarifiwa kwamba fomu za kugombea nafasi ya Ubunge wa *NEC* zipo tayari zinapatikana Ofisi ya CCM katika ofisi ya Wawakilishi, fomu zinaanza kutolewa leo tarehe 10/11/2020 hadi tarehe 12/11/2020. Kwa hiyo, wale wote ambao wangependa kugombea nafasi hizo wataelekea huko kwenye Afisi Kuu ya CCM na maelezo yanayohusiana na jambo hilo watayapata huko kwa ukamilifu.

Baada ya hapo, sasa naomba nimwite Katibu kwa shughuli inayofuata.

**Katibu**: Mhe. Spika, naomba kutoa taarifa kwako na kwa Baraza lako tukufu kwamba shughuli zote tulizozipanga leo zimekamilika.

**Mhe. Spika:** Ahsante Katibu. Sasa kwa vile shughuli zote zilizopo kwenye *order paper* zimekamilika naomba kuliakhirisha Baraza mpaka kesho siku ya Jumatano tarehe 11/11/2020 saa 8:00 mchana kama ambavyo hoja imetolewa. Ahsanteni Waheshimiwa.

*(Saa 8:25 mchana Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 11/11/2020 saa 8:00 mchana)*